SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.24 NO. 1 2025
DOI: 10.51984/JOHS.V24I1.3704

مجلة جامعة سبها للعلوم الإنسانية
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: http://www.sebhau.edu.ly/journal/johs

# UCHAMBUZI WA FASIHI ZA KIFUNGWA: MFANO KUTOKA HAINI

*Ismahan Abulkasim Issa , Jalgham Abuazuom Emhemed Ali

Department of African Languages and Studies, Faculty of Languages, Sebha University

**Maneno muhimu:**
Fasihi
Nadharia
Ufungwa
Jela
kazi.

**MUHTASARI**

Makala hii inahusu uchambuzi wa fasihi za ufungwa ambazo zimehakiiwa kwa mkabala wa pendekezwa wa nadharia ya ufungwa. Ufungwa kama nadharia pendekezwa ya kuhakikia kazi za kifasihi za Ufungwa. Dhana ya Ufungwa hufasiliwa kama hali ya mtu kuwekwa jela akitumikia kifungo. Fasihi ya Ufungwa ni dhana ngeni ya kifasihi inayorejelea maandiko au kazi zote zinazohusu maisha ya jela au mahabusu. Aghalabu kazi za ufungwa huhusishwa na miktadha ya maisha ya mwandishi wa kazi husika.

Kimazoea nadharia huendelea kutumika kuhakiki kazi za kifasihi kwa muda mrefu hata kama nadharia hiyo inapwaya. Hivyo, kwa upungufu huo mhakiki hujikuta akitumia nadharia zaidi ya moja kuhakiki kazi husika ili kuweza kukidhi malengo yake. Hata hivyo, hali hii inapaswa kubadilika kutokana na kasi na mitindo na kumbo mpya za kifasihi zinazoibuka hususani Fasihi ya Ufungwa. Kutokana na mabadiliko haya nadharia kongwe hujikuta hazina budi kupisha nadharia mpya ili ziendelee kuhakiki kazi mbalimbali zinazoibuka.

Oswald, anaona kazi za ufungwa zinaweza kuhakikiwa kwa nadharia ya Kuwako" (Existentialism), Uhistoria Mpya", na „Elimu Mitindo" Pamoja na muongozo huu lakini tunaona bado nadharia hizo pia hazijitoshelezi kuhakiki kazi ya ufungwa kwa ujumla wake. Badala yake, zitajikita katika kuchambua tukio mojamoja. Hivyo, tunaona jinsi tunavyopata shida tunapotakiwa kuchambua kazi za ufungwa. Hatuwezi kuongozwa na nadharia moja ama mbili zikatosheleza, bali tutajikita katika kutumia mzigo wa nadharia katika kuhakikia kazi moja. Kwa upungufu huu, makala hii itajaribu kupata suluhisho la nadharia ambayo ingeweza kuhakiki kazi za ufungwa kwa jumla pasi na kutumia rundo la nadharia katika kazi moja. Makala hii itafafanua jinsi nadharia pendekezwa ya Ufungwa itakavyojitosheleza kuhakiki kazi za ufungwa ikidondoa mihimili ya nadharia hiyo na matumizi yake.

# تحليل الأدب النهائي مثال من هايني

*أسمهان أبوالقاسم عيسى و جلغم أبو عزوم امحمد علي

قسم اللغات والدراسات الأفريقية، كلية اللغات، جامعة سبها

**الكلمات المفتاحية:**
الأدب
النظرية
السجن
السجن
العمل.

**الملخص**

هذه المقالة تختص بدراسة وتحليل أدبيات السجون التي تحاكي للنهج المقترح لنظرية السجون. السجن كنظرية مقترحة لضمان تقييم الأعمال الأدبية. يمكن ان يعرف مفهوم السجن بأنه وضع الشخص في السجن أثناء فترة العقوبة، وأدب السجون هو مفهوم أدبي أجنبي يشير إلى كافة الكتابات أو الأعمال التي تختص بحياة السجون أو السجناء، وغالبًا ما تختص اعمال السجون بسياقات ومقتضيات حياة مؤلف العمل. في العادة يستمر استخدام النظرية لتقييم الأعمال الأدبية لفترة طويلة حتى لو تم تهالك هذه النظرية وبالتالي وبسبب هذا القصور يجد الكاتب نفسه يستخدم أكثر من نظرية للتقييم ومراجعة العمل المعني ليستطيع ان يحقق أهدافه لكن هذا الوضع يجب أن يتغير من خلال السرعة والأساليب والأنواع الأدبية الجديدة التي تظهر وخاصة أدب السجون. ونتيجة لهذه التغييرات تجد النظريات القديمة نفسها مضطرة إلى تمرير نظريات جديدة من أجل تطوير تقييم الأعمال الناشئة المختلفة. ويرى اوسوالد أنه يمكن تقييم اعمال السجن من خلال نظرية الوجود (الوجودية) والتاريخ الجديد و"أساليب التعليم" من خلال هذا الدليل ولكننا لا نزال نرى أن هذه النظريات ليست كافية لمراجعة وتقييم اعمال السجون ككل وبدلا من ذلك سوف يركزون على تحليل الأحداث الفردية وهكذا نرى كيف يتم مواجهة المشاكل عندما يتعين علينا تحليل أعمال السجون ولا يمكننا أن نسترشد بنظرية أو اثنتين إذا كانتا

*Corresponding author:
E-mail addresses: asm.masoud@sebhau.edu.ly, ( J. A. E. Ali) jal.ali@sebhau.edu.ly
*Article History: Received 01 December 2024 - Received in revised form 09 May 2025 - Accepted 30 June 2025*

كافيتين، ولكننا سنركز على استخدام عبء النظرية في تقييم عمل واحد ومع هذا القصور فهذه المقالة تحاول إيجاد حل نظري يمكنه تقييم اعمال السجون اجمالا. سنشرح في هذه المقالة كيف ستكون نظرية السجن المقترحة كافية لتقييم أعمال السجون واستخلاص أركان النظرية وتطبيقها.

**Tngulizi:**

Dhana ya jela sio jambo geni katika jamii. Jamii nyingi iliifahamu jela kuwa ni sehemu ya ufundishaji wa nidhamu kwa waliokosea. Adhabu ilitumika kama njia ya kufundisha mtu nidhamu. Foucult mwanafilosofia na mwanahistoria kutoka ufaransa ndiye wa kwanza kujadili nafasi ya jela katika jamii. Foucult (1979) alieleza kwa mara ya kwanza kuwa dhana ya jela hapo awali ilikuwa ni kutokana na haja ya kupeleleza jambo ambalo lilifungwa nyakati za ugonjwa wa tauni ili kulinda jamii kutokana na ugonjwa huo. Katika hali kama hii wanajamii walidhibitiwa ili wasitengamane na watu wengine (waathirika). Baada ya muda dhana ya jela ilipata mtazamo mwengine wa kumrekebisha mtu tabia na hulka zake kupitia mazoezi na kazi. Kawaida jamii imejengwa kwa msingi ya uhuru ilihali jela imejengwa kwa msingi wa kumpokonya mtu uhuru huo, kwa kufanya hivyo ikiwa ni kumuadhibu mtu au mwanajamii huyo.

Kwa mujibu wa Foucult anapendekeza kuwa jela iwe na majukumu kama vile:

- Kumtenga mhalifu kutokana na mwanajamii wengine na ulimwengu kwa jumla.
- Tabia na hulka zake zinarkebishwa kupitia kudhibiti saa, maisha na kazi katika jela.
- Jela huamua adhabu kwa kosa la mfungwa, na kiwango cha adhabu kina amuliwa na jela sio makosa ya mfungwa.
- Jela iwe na mantiki fulani, kuwe na uhusianao kati ya kosa na nidhamu.
- Kuwe na kubadili au kurekebisha adhabu zisiwe ni adhabu zisizobadilika kulingana na wakati, makosa makubwa yawe na adhabu ndefu.
- Nidhamu ktk jela ielekezwe kwa wafungwa na wanajamii wengine pia. Yaani adhabu itolewwe hadharani wengine wakitazama pia ndio iwe funzo kwa jamii nzima.

**1.1 Historia ya Fasihi ya Ufungwa**

Kipengele hiki kinafafanua historia ya Fasihi ya Ufungwa. Historia itaelekezwa katika nchi za Ulaya, Afrika, na Afrika Mashariki.

**1.1.1 Fasihi ya Ufungwa katika Mawanda ya Kiulimwengu**

Ni vigumu kupata historia ya Fasihi ya Ufungwa ikiwa katika mtiririko mzuri. Hata hivyo, Franklin (1998) anadai kuwa historia ya Fasihi ya Ufungwa inaweza kuangaliwa kuanza katika miaka ya 524 BK huko Ulaya. Fasihi ya Ufungwa ilishika kasi katika nchi za Ulaya baada ya Miguel de Cervantes kutoka kifungoni katika miaka ya 1605 BK. Cervantes aliishi maisha ya kifungoni kati ya mwaka 1575 na 1580. Baada ya kazi ya Cervantes, kazi nyingi za ufungwa zilishamiri miaka ya 1900. Kwa mfano, Cummings katika mwaka 1922 aliandika Riwaya yake iliyoitwa *The Enormous Room* akiwa na Wafaransa wakati wa Vita Kuu vya Kwanza vya Dunia. Adolf Hitler pia aliandika historia yake pamoja na itikadi yake ya kisiasa katika kitabu chake alichokiita *Mein Kampf* baada ya kufungwa katika bwalo la Beer Hall Putsch mwaka 1923. Mwanafalsafa wa Kikomunisti wa Italia Antonio Gramsci aliandika sehemu kubwa ya kazi yake ya Fasihi akiwa jela baada ya kufungwa na Mussollin miaka ya 1930.

Sehemu kubwa ya kazi za Fasihi ya Ufungwa zilikuwa katika muundo wa barua, historia fupi na mashairi. Kwa upande wa riwaya, kazi chache ziliandikwa. Hii ilitokana na mazingira magumu ya maisha ya gerezani. Maisha magumu hayo ni kama vile, mateso, hali ngumu ya maisha na adhabu kali wazipatazo waandishi kama wafungwa wawapo magerezani. Aidha, kwa upande wa Marekani, kazi nyingi za ufungwa ziliandikwa katika karne ya 20. Kazi hizi ni kama vile *My Life in Prison* ya Donald Lowrie, Cell Mate ya Agnes Smedley, *Crime and Criminals* ya Kate Richards O'Hare, na The Autobiography of Malcolm X ya Malcolm X. Nyingine ni *Sing Soft Sing Loud* ya Patricia McConnel, na *AIDS: The View from a Prison Cell* ya Dannie Martin. (Franklin, 1998).

**1.1.2. Fasihi ya Ufungwa katika Mawanda ya Bara la Afrika**

Fasihi ya Ufungwa inajitokeza sana katika nchi ya Afrika ya Kusini. Hii inatokana na historia ya utawala wa kibaguzi na mapigano nchini humo. Hali hii ilisababisha maisha ya Waafrika wengi kuwa ya ufungwa. Kazi maarufu ya Fasihi ya Ufungwa ambayo ndiyo inasadikiwa kuwa "baba" wa kazi za ufungwa katika Afrika Kusini na hata Afrika ni riwaya ya *Cold Stone Jug*. Riwaya hii iliandikwa na Herman Charles Bosman mwaka 1949 na kuchapishwa upya mwaka 1999 chini ya uhariri wa Stephen Gray.(Bosman ni Mwafrika aliyezaliwa tarehe 3/2/1905 mjini Cape Town nchini Afrika Kusini na kufariki tarehe 14/10/1951. Aliwahi kuhukumiwa kunyongwa na kufungwa katika gereza Kuu la Pritoria kwa kosa la kumuua kaka yake).

Bosman aliandika riwaya hii miaka mingi baada ya kutoka jela. Kazi zingine maarufu za ufungwa nchini Afrika Kusini ni pamoja na kazi ya Ruth First ambaye aliandika historia ya kukamatwa kwake mwaka 1965, Albie Sachs aliyeandika The Jail Diary of Albie Sachs mwaka 1966 na Hugh Lewin aliyeandika Bandiet mwaka 1974 (Oswald, 2005). Aidha, tunapotaja kazi zilizojitokeza nchini Afrika Kusini, pamoja na kazi hii ya Bosman, pia hatuwezi kuitenga kazi ya Nelson Mandela ya *The Long Walk to Freedom* na Alex La Guma kwa kazi yake ya *The Stone Country* ambazo nazo zimeleta mchango mkubwa katika Fasihi ya Ufungwa.

Nchini Nigeria, Fasihi ya Ufungwa ilishika hatamu miaka ya 1960, baada ya vita vya wenyewe kwa wenyewe vya mwaka 1967. Mwaka huo watu wengi walikamatwa na kuswekwa rumande na Serikali ya Mapinduzi ya Yakubu Gowon kwa sababu za kisiasa. Miongoni mwa watu waliokamatwa ni pamoja na mwandishi maarufu wa Nigeria Wole Soyinka2. Soyinka ndiye mwanzilishi wa maandiko ya ufungwa nchini Nigeria. Mwandishi huyu ameweza kuandika kazi za ufungwa kutoka katika tanzu za ushairi na barua. Miongoni mwa kazi hizo ni pamoja na diwani ya ushairi aliyoiita Poems from Prison aliyoichapa mwaka 1969. Kazi hii inasemekana aliiandika akiwa gerezani na mara baada ya kutoka aliweza kuchapisha mashairi hayo. Pia katika utanzu wa barua, Soyinka aliandika The Man Died: Prison Notes. Kwa utunzi wake wa kazi mbalimbali za Fasihi, Soyinka aliweza kuwa Mwafrika wa kwanza kutunukiwa tuzo ya heshima ya Fasihi mwaka 1986. (Soyinka alizaliwa tarehe 13/7/1934 katika familia ya ki-Yoruba huko Abeokuta nchini Nigeria. Ni mwandishi na Profesa wa tamthiliya za kimashairi na riwaya nchini Nigeria. Ni Mwafrika wa kwanza kutunukiwa tuzo ya Nobel ya Fasihi. Aliwahi kufungwa miezi 22 kwa sababu za kisiasa).

Pamoja na hao, Wanjiru (2010) anamtaja Kwame Nkurumah, rais wa kwanza wa Ghana ambaye aliandika tawasifu yake akiwa katika gereza la Ngome ya James huko Ghana wakati akipigania uhuru wa taifa lake chini ya utawala wa Waingereza. Mwingine wa Ghana ni Kofi Awoonor. Nchini Malawi ni Jack Mapanje kwa diwani yake ya *Of Chameleons* and *Gods* alilochapisha baada ya kutoka kifungoni. Na nchi ya Angola anatajwa Agostino Neto kuwa ni miongoni mwa waandishi wa ufungwa aliyeandika diwani ya mashairi yaliyoitwa *Sacred Hope.*

Aidha, Wanjiru anawataja wengine katika nchi zingine kama vile Dennis Brutus, aliyeandika Letters to Martha, Sherif Hatata na Nawal El Saadawi kutoka Misri. Pia Zainab Alghazali katika riwaya yake aliyoiita *Matukio katika Maisha Yangu* iliyoandikwa kwa lugha ya Kiarabu kama vile *Ayyaam Min Hayaatt* na kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na kwa lugha ya Kiingereza kama *Days From my Life,* anaelezea maisha yake alipokuwa gerezani nchini Misri na adhabu alizozipata.

**1.1.3 Fasihi ya Ufungwa katika Mawanda ya Ukanda wa Afrika Mashariki**

Tukiangazia Fasihi ya Ufungwa nchini Kenya, tunaona rais wa Kenya, Jomo Kenyatta, ndiye anayechimuza kazi za Ufungwa nchini Kenya kwa kazi yake ya *Facing Mount Kenya* aliyoiandika mwaka 1938. Kazi hii inafungua milango katika kuzibainisha kazi za Ufungwa nchini humo. Hata hivyo, kazi hiyo haikuwa ya ufungwa kwa asilimia mia, bali ufungwa katika kazi hiyo umeelezwa kwa namna ya kificho zaidi.

Aidha, Wanjiru (2010) anamtaja Kariuki kuwa ni Mkenya wa kwanza kuandika maisha kuhusu jela katika kazi isiyo ya kibunilizi katika kipindi cha ukoloni. Kazi yake hiyo aliita *Mau Mau in Detention* aliyoiandika mwaka 1963. Wengine waliomfuata ni kama vile Gakaara wa Wanjiru aliyeandika kitabu kiitwacho Mwandishi wa Mau Mau Ithamerio-ine (Mau Mau Author in Detention).

Baada ya uhuru, Wanjiru anaona kuwa Ngugi wa Thiong'o ndiye aliyeshika kijiti katika usanaji wa kazi za ufungwa kwa kazi yake ya Detained: *A Writer's Prison Diary* (1977) na *Shetani Msalabani* (1978). Wengine waliotoa mchango katika uga huu ni pamoja na Maina wa Kinyatti aliyeandika mashairi ya *A Season of Blood*: *Poems from Kenyan Prison* (1995), Kenya -*A Prison Notebook* (1996) na *Mother Africa*, Koigi wa Wamwere, Wanyiri Kihoro *Never Say Die*, Wahome Mutahi naye aliandika *Three Days on the Cross* na *Jail Bugs*. Pia, Wahome aliandika *Three Days on the Cross*. Waandishi wengine nchini Kenya ni John Kiriamiti aliyeandika *My Life in Crime*, Kiggia Kimani aliyeandika *Prison is Not a Holiday Camp*, Charles Githae kwa kazi yake ya Comrade Inmate, Karuga Wanadai kwa kazi yake ya *Mayor in Prison* na Benjamin Garth Bundeh *Birds of Kamiti*.

Waandishi wengine waliojitokeza katika Afrika Mashariki baada ya uhuru ni Abdillatif Abdallah aliyeandika mashairi akiwa gerezani akitumia karatasi za chooni. Diwani yake hiyo aliita *Sauti ya Dhiki*. Kazi hiyo ya Abdillatif Abdallah ndiyo iliyofungua mlango wa maandiko ya ufungwa ya Kiswahili nchini Kenya baada ya uhuru.

Nchini Tanzania, bunilizi za Ufungwa zimeanza kutumika miaka ya 1990; mwanzilishi wake akiwa ni Maulid Haji kupitia riwaya yake ya Umleavyo, (Madumulla, 2009:58). Tangu miaka ya 1990 Maulid Haji alipotoa kazi yake ya Umleavyo tunamuona mwandishi mwingine aitwaye Adam Shafi katika riwaya yake ya Haini iliyochapishwa mwaka 2003, nayo ikisawiri maisha ya jela.

Licha ya kazi hizi mbili za ufungwa za waandishi lengwa, pia tumebaini kazi nyingine zinazohusu ufungwa katika tanzu mbalimbali. Kazi hizo ni pamoja na kazi ya kitawasifu ya Kamara Kusupa iitwayo Maisha yangu Gerezani: Siku 1888 za Mateso iliyochapishwa mwaka 2014. Tawasifu nyingine ni ya Ben R. Mtobwa iitwayo Mhariri Msalabani ya mwaka 2003. Pamoja na kazi hizi pia zipo baadhi ya kazi za mwandishi Ibrahim Gama ambaye anaugusia ufungwa kama motifu mojawapo ijengayo kazi zake. Kazi zake hizo ni pamoja na Barua Kutoka Jela na Mpita Njia. Nchini Tanzania kazi iliyoandikwa na Amani Thani Fairooz3 akaiita Ukweli ni Huu (Kuusuta Uwongo) inajipambanua kuwa ni miongoni mwa maandiko ya ufungwa. Kazi hii inaelezea maisha na masahibu yaliyomkuta mwandishi Amani Thani katika uhai wake. Ndani yake imekitwa historia ya siasa ya Zanzibar, suala la mapinduzi ya Zanzibar na madhara yake kwa raia wa Zanzibar, na mwisho mwandishi anasimulia mazao ya mapinduzi ya Zanzibar kwake na kwa raia wengine wa Zanzibar. Aidha, mwandishi anasimulia jinsi mapinduzi yalivyowatesa na kuwaingiza jela raia wasio na hatia. Katika kazi yake hiyo anaelezea maisha waliyokuwa wanaishi jela na madhila waliyoyapitia wakiwa katika gereza la Kiinuamiguu, Langoni na Kwa Ba Mkwe huko Zanzibar.

Katika Fasihi simulizi pia tunakutana na kazi mbalimbali zilizosanwa na Watanzania zenye uelekeo wa ufungwa, ikiwa ni pamoja na nyimbo na filamu. Nyimbo ambazo zinazohusu ufungwa ni pamoja na Nipe Ripoti wa Tunda Man, Toka Nitoke Jela wa Spake, Mikononi mwa

Polisi wa Sugu, Imekaa Vibaya wa Kal P Bange Bange wa Twenty Percenty, Bora Nirudi Jela wa Husein Machozi, Jela wa FM Academia na Wanaokwenda Jela wa Insipector Haroon . Na katika filamu tunakutana na filamu kama vile Taqwa iliyotungwa na Issa Kiparamoto, Kimenuka iliyotungwa na Jimmy Mafufu, Mikono Salama iliyotungwa na Irene Sanga na Mahabusu ilitungwa na Richard Mzirai.

Kazi zote tulizozitaja kwa njia moja au nyingine zimekuwa zikiangazia hali halisi ya wafungwa, maisha katika jela, adhabu na mateso mengine yanajitokeza jelani. Aidha shida wanazopitia jamaa wa karibu kama vile wake, wazazi, watoto na hata marafiki wanaouhusiana na mtuhumiwa au mshtakiwa aliyoko gerazni. Waandishi wa kazi hizi za kifungwa wamekuwa wakijaribi kutoa hisia zao na ujumbe kwa jamii kufahamu ale yanajiri ndani ya kuta za jela pengine wengi wa watu wa kawaida hawayafahamu. Katika kazi za fasihi ya Kiswahili zinazohusu ufungwa bado hazijapata nadharia faafu kutumika kuhakiki kazi hizo. Kutokana na hilo ndio tunapendekeza nadharia hii ya fungwa (N.U) iweze kutumika kuhakiki kazi za kifungwa kwa kurejelea mihimi ifutayao.

**2.0 Dhana ya Nadharia**

Wafula na Njogu (2007) Wanafasili nadharia kama istilahi ya kijumla inayomaanisha miongozo inayomwelekeza msomaji wa kazi ya Fasihi kuifahamu kazi ya fasihi katika vipengele vyake vyote. Ni maelezo ya jambo yanayofungamana na vigezo vilivyowekwa au vinavyozalika kutokana na majaribio ya jambo hilo.

**2.1. Namna ya Kupata Nadharia**

Nadharia huweza kupatikana kwa njia anuai kama zinavyoelezwa na Wafula na Njogu (2007). Mojawapo ya njia wanazozijadili za kuunda nadharia ni pamoja na jopo la wataalamu au mtu binafsi aliyesoma kwa makini kazi ya fasihi. Wanasema kuwa, kwa hali hii ya pili ya upatikanaji wa nadharia hutokea ikiwa msomaji wa kazi husika hana marejeleo maalumu yatakayomsaidia kusoma kazi ya fasihi. Hivyo anapaswa kujitafutia vigezo vitakavyo mwezesha kuisoma kazi ya fasihi kwa utaratibu maalumu na kuainisha iwapo kazi hiyo imefaulu au haijafaulu.

Namna ya pili ya kuipata nadharia kama ilivyojadiliwa na Njogu na Wafula, ndiyo inayotushawishi kujaribu kutafutia vigezo vya kuhakiki kazi zinazohusiana na ufungwa. Baada ya kuhangaika kutafuta nadharia inayofaa zaidi katika kuhakikia kazi za ufungwa na kujiridhisha kuwa nadharia nyingi yazo zinapwaya, mwandishi anajaribu kuuunda „Nadharia ya Ufungwa‟ itakayojaribu kuziba pengo hilo.

**3.0 Mihimili au Mikabala ya Nadharia Pendekezwa ya Ufungwa**

Oswald (2005) anatoa dira juu ya nadharia zinazopaswa kuhakikia kazi za ufungwa akimakinikia kazi ya Cold Stone Jug ya Bosman. Anaona kuwa kazi hiyo ingeweza kuhakikiwa kwa nadharia anuwai, ikiwemo nadharia ya „Kuwako‟ (Existentialism), „Uhistoria Mpya‟, na „Elimu Mitindo‟. Anaona kuwa nadharia hizo zinaweza zikatumika kuhakikia kazi za ufungwa, ikiwemo kazi ya Cold Stone Jug. Pamoja na muongozo huu wa Oswald juu ya kutoa dira kuhusu nadharia ya kuhakikia kazi za ufungwa, lakini bado nadharia hizo pia hazijitoshelezi kuhakiki kazi ya ufungwa yote. Badala yake, itajikita katika kuchambua tukio mojamoja. Kwa upungufu huu, mtafiti anajaribu kupata suluhisho la nadharia ambayo ingeweza kuhakiki kazi za ufungwa kwa jumla pasi na kutumia rundo la nadharia katika kazi moja.

Ili kuijaribia nadharia hii mchambuzi wa kazi za ufungwa anapaswa kujiegemeza katika misingi ifuatayo:

i. Ujela ikiwa ndio mhimili mkuu wa kazi ya ufungwa.

Kazi ya kifungwa lazima izungumzie maisha ya magereza. Mhakiki hapa aangazie jinsi wafungwa wanavyoishi jela ndani ya kazi husika kimandhari na kivitendo. Je, maisha ya jela yanayosawiriwa katika kazi husika husawiri raha au utanzia; unyanyasaji wa kijinsia; ubabe dhidi ya wafungwa kwa wafungwa; polisi wa magereza dhidi ya wafungwa; chakula; malazi; kazi; tabia n.k.

ii. Uso huru wa wahusika wa kazi husika kijamii, kiutamaduni, kiuchumi, kiakili, kifikra ama kimwili.

Mhakiki achunguze hali zote zinaompitikia muhusika katika kazi za kifungwa ikiwemo masuala ya kijamii, kiuchumi, kiakili n.k.

iii. Maisha ya mwandishi na zao la kazi yake.

Kazi husika lazima iwe ni zao lililojengwa na miktadha ya maisha ya mwandishi.

Kama inavyofahamika kuwa fasihi ni zao la jamii. Mwandishi yeyote wa kazi ya fasihi huandika kile alichokiona, kisikia, kupitikia, kusimuliwa n.k. Kadhalika hali hii tunaikuta sana katika kazi za fasihi za kifungwa kama tulivyoona katika historia ya kazi za ufungwa hapo juu. Hivyo mhakiki anatarajiwa kuhusianisha maisha ya mwandishi nakazi yake.

iv. Matumizi ya lugha na Istilahi za jela.

Mhakiki amakinikie kuchunguza kauli ya mwandishi na zile kauli awabebeshazo wahusika. Lengo ni kubaini kama kuna lugha ya ukali, amri, matusi, vitisho, dharau, nasaha, lugha ya upole, kejeli, chuki, kisasi na istilahi zitumikazo jela.

v. Hukumu juu ya mtuhumiwa na mshatakiwa kwa wafungwa.

Mhakiki achunguze sababu za wafungwa kuwepo hapo jela. Achunguze asili ya hukumu anayopatiwa mtuhumiwa na mwisho wa kifungo chake. Je, wafungwa waliopo jela, wote wapo kwa ajili ya makosa yao? Je, ni watuhumiwa au washtakiwa? Je, wanahatia ya kupelekwa jela? Je, uchunguzi ulifanyika sawa hadi kuhukumiwa

kifungu? Maswali kama haya yatamuwezesha mhakiki aweze kujua hasa chanzo na sababu za mfungwa kuweka jela. Ili kubaini haki na batili ya kifungo hicho na mwenendo wa kesi uliotumika kutoa hukumu.

vi. Mipaka ya adhabu na kifungo cha mfungwa na athari zake.

Ni muhimu kuchunguza asili ya hukumu anayopatiwa mtuhumiwa na mwisho wa kifungo chake. Ili kubaini haki na batili ya kifungo hicho na mwenendo wa kesi uliotumika kutoa hukumu. Maelezo ya ziada, Adhabu zitolewazo kwa wafungwa zimekuwa hazina mipaka kwao. Adhabu za wafungwa wanazopewa zimekuwa si kwa wafungwa tu bali zimekuwa zikiwafikia hadi watu wake wa karibu kama kama vile : mke/ mume, watoto, wazazi , ndugu n.k.

**2.3 Uchambuzi wa kazi za fasihi za kifungwa kwa mkabala wa Nadharia ya Ufungwa: Mfano *Haini***

*Haini* ni moja ya kazi ya fasihi ya kifungwa ilioyondikwa na Shafi Adam Shafi. Kwa kurejelea mihili pendekezwa hapo juu tunaona jinsi gani mwandishi Adam Shafi anavyoweza kusawiri maisha ya gereza tangu watuhumiwa wanasakwa waliokuwemo na wasiokuwemo, kwa kosa la kuuliwa kigogo, maisha yao ya jela na hadi hukumu yao. Mwandishi anaanza kukitafuta chanzo cha ufungwa kisha watuhumiwa wanatafutwa na kukamatwa. Halafu anaonesha maisha ya magereza na mwisho anaeleza jinsi hukumu ilivyotolewa. Dondoo zifuatazo zinajieleza kuhusu mwandishi anavyosawiri maisha ya jela.

Siyo ile nyama wanayoletewa kutoka kumbakumba. Nyama chapwa, iliyochemshwa ikatolewa supu zaidi ya mara nne. Supu ya askari, supu ya wapishi, supu ya kofia nyeusi na mtaimbo wa mwisho ndio supu yao. Supu chururu na chumvi ya kurashia rashia tu.

Pia, Shafi anayasawiri jinsi hali ya ulalaji wa magereza katika (uk.16) kama ifuataavyo:

Saa ngapi wanaleta magodoro? Aliuliza, ki-lillah, hakukusudia mzaha wala kejeli.

.... Unaiona hii sakafu usiyotaka kuigusa? Hiki ndiyo kitanda chako nd‟o godoro lako, nd‟o mto wako, nd‟o shuka yako ya kujifunika.”

Enh! alishtuka. Manake! Manake!

Tukichunguza kwa makini maelezo hayo hapo tunaona ni jinsi watuhumiwa hawa wanavyopatwa na shida kuanzia chakula wanachopewa, malazi yao na lugha ya vitisho kama hiyo. Katika hali halisi hawa si wafungwa wangali ni watuhumiwa. Lakini tunaona jinsi gani wanvyoteswa na kubughudhiwa. Hawaruhusiwi kujitetea wala hakuna mtetezi wa kuwatetea. Pengine hii ndiyo hali inayokumba watuhumiwa walio wengi magerezani. Hivyo kutokana na hali kama hii inayotendewa watuhumiwa inawalazimu vitengo husika wanaohusiana na majukumu ya wafungwa kupewa haki zao zinazostahili kama binaadamu wengine sio kuchukuliwa kama wanyama au viumbe wasio haki.

Katika mhimili mwengine tunaona jinsi mwandishi anavyousawiri uso uhuru wa wahusika wake kijamii, kiutamaduni, kiuchumi, kifikra na kimwili. Anaonesha jinsi uhuru ulivyobanmwa kwa wahusika wake. Kwa mfano, mhusika Khadija mke wa Hamza tunaona anafungwa kijamii, pale anapokosa uhuru wa kuishi na jamii inayomzunguka kwa sababu tu husemwa na wanajamii kwa kuwa mumewe Hamza katuhumiwa kesi ya uhaini. Kiutamaduni Khadija ana ufungwa wa kimapenzi lakini anashindwa kuwa huru kufanya mapenzi nje ya ndoa yake kutakana na tamaduni za kiimani zinazomzunguka. Kiuchumi Khadija na wanajamii kwa ujumla wanafungwa na mikatale ya uchumi iliyowazunguka. Tunaona jinsi bidhaa mbalimbali zinavyokuwa shida katika kupatikana kwake ijapokuwa pesa za kununullia zipo. Lakini mwananchi hana uhuru wa kufanya matumizi katika muda autakao. Bidhaa huuzwa katika siku mahsusi ya wiki. Tunayaona haya kaatika ukurasa wa 140.

Maisha ya mwandishi na zao la kazi yake huu ni mhimili ambao unaangazia maisha halisi ya mwandishi yanalandana kwa asilimia kubwa na maisha ya Hamza katika Haini. Tunaona kuna athari kati ya maisha ya mwandishi na utunzi wake. Historia ya Shafi inaonesha aliwahi kuishi gerezani huko Zanzibar kwa tuhuma za kumuua rais Karume. Kwa hiyo tunaona kazi hii ya Haini ni tokeo la kufungwa kwake.

Katika riwaya ya Haini tunaona matumizi ya lugha na Istilahi za jela kama mhimili mwengine unavyojitokeza waziwazi. Kwa mfano lugha anayoitumia mwandishi kupitia wahusika wake ni kali iliyojaa kejeli, matusi na manung‟uniko. Mwandishi anasema:

Ambar ni mwanasheria aliyebobea. Ana digrii mbili za sheria kutoka Chuo kikuu cha Lumumba cha nchini Moscow. Kwa mfumo mpya wa mahakama za wananchi, Mwanasheria kama Faraji walionekana kama mabazazi tu wenye kudanganya watu. Faraji kwa hivyo alikuwa hana kazi…

“Kesi, kesi,” alikejeli Sururu.“Mahakimu wenyewe wale? Wengine wauza samaki wameokotwa sokoni? Pana kesi hapo? Aliuliza Sururu… (uk 107-108).

Kiti cha mkono wa kulia wa upande wa washtakiwa amekaa Pandu, mtu asiyewahi kutia mguu wake ndani ya darasa la skuli, mbumbumbu wa kutupwa, mwuza samaki katika soko la kwa Hajitumbo.

Mkono wa kushoto amekaa Jongo. Akisifika kwa kuendesha baiskeli mbio wakati wa ujana wake alipokuwa akiuza maziwa...

Kiti cha katikati amekaa Musadiq. Inaonesha dhahiri kwamba yeye ndiye kiongozi wa jopo lile la mahakimu. Yeye ni mwalimu wa chuoni, mchana anasomesha Kurani, usiku anasomesha darsa...

Kigogo mwenyewe pale alipozivunja mahakama zote za mahakimu wa kuvaa majuba na nywele za bandia, akafuta na utaratibu wote wa kimahakama wa watetezi wanaovaa makoti meusi na tai. Akawaita mahakimu na mawakili wa Mahakama hizo ni malaghai, mabingwa wa kuugeuza ukweli ukawa uongo na uongo ukawa ukweli. Akaunda mahakama zake mwenyewe… Na ndio hawa waliopo hapa mwuza samaki, muuza maziwa na mwalimu wa chuoni…(uk 232).

Shafi anatumia kejeli kuusemanga mfuumo wa Mahakama na viongozi waliopewa wadhifa wa kuhukumu kesi hali ya kuwa hawana taaluma ya sheria. Hapa mtunzi anakejeli mfumo wa serikali kwa jumla, kwani sekta nyeti zimeonekana kukaliwa na watu wasio na sifa, na badala yake, watu wenye taaluma husika wakihaha barabarani bila ya kazi.

Hukumu juu ya mtuhumiwa na mshatakiwa kwa wafungwa, kwa mwongozo wa mhimili huu tunaona jinsi kosa, hukumu, adhabu walizopewa wahaini inavyoendana au kutofautiana kulingana na kosa lililofanyika. Tunaona wauaji walivyosombwa nakupelekwa gereza la Kinoamiguu, walioonekana kweli wamehusika na mauaji walihukumiwa kunyongwa, wengine walihukumiwa vifungo virefu. Licha ya hayo tunaona pia jinsi wategemezi walivyoathirika na hukumu hizo. Tunaona jinsi Khadija mke wa Hamza alivyohangaika kwa waganga ili mumewe apate nusra ya kifungo. Aidha, mwenendo kesi uhaini inasawiriwa ni ya kibaguzi iliyoshitadi ubabe na ushahidi wa kubabatizwa na viongozi wa juu wenye mabavu ambao kwa namna moja ama nyingine ndiyo waliohusika kumuua kigogo.

**3.0 Hitimisho**

Huu ni mfano mmoja wa kazi za kifasihi za kifungwa inavyoweza kuhakikiwa na Nadharia ya Ufungwa. Hivyo basi, kupitia mihimili hii bila shaka kazi ya ufungwa inapohakikiwa itakuwa imekidhi matakwa ya kazi husika pasi na kuhitaji nadharia mbadala ili kutosheleza ama kusaidia ama kuziba mapengo yaliyoachwa na nadharia husika ambayo haikujitosheleza. Aidha, nadharia ya Ufungwa inaweza kutumika katika mambo ya kijamii yanayohusu jela katika jamii. Mtafiti anatoa wito kwa watafiti wengine kujaribia nadharia ya ufungwa kama ilivyowekewa misingi na mtafiti hapo juu.

**MAREJELEO**


Al-Ghazar, Z. (1996), *Matukio Katika Maisha Yangu*, Islamic Propergation Centre, Dar es Salaam, Tanzania.

Broemmel, M.C. (haujatajwa), “Definition of Incarceration” [hhtp://www.ehow.com/about-5127510-Definition- Incarceration] imepitiwa tarehe 12/11/2015 saa 6:23 mchana.

Diegner, L. (2011), “Mazungumzo na Adam Shafi juu ya Uandishi wake wa Riwaya: Adam Shafi & Lutz Diegner”, Swahili Forum 18 (37-68).

Fairooz, A.T. (1995), Ukweli ni Huu (Kuusuta Uwongo), Kimesomwa toka [http://www.fortunecity.com/victorian/abbey/313/ukweli.html], Kimepitiwa tarehe 19/4/2016.

Haj, Maulid. (1990), Umleavyo, Oxford University Press, Nairobi Kenya.

Karugendo, P. (2013), "Uhakiki wa Kitabu cha *Haini*" [http://www.karugendo.net/2013/05/normal-0-false-false-false-en-us-x-none_2672. html]. Imepitiwa tarehe 12, Sep, 2015.

Kusupa, K. (2014), *Maisha Yangu Gerezani: Simulizi ya Siku 1888*, Karlimjeer, Dar es Salaam, Tanzania.

Mdee, J.S. na Wenzake (2011), *Kamusi ya Karne ya 21*, Longhorn Publishers, Dar es Salaam, Tanzania.

Mdundo, M.O. (1999), *Masimulizi ya Sheikh Thabit Kombo Jecha*, DUP Ltd, Dar es Salaam, Tanzania.

Msokile, M. (1993), *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*, East African Education Publishers, Nairobi.

Mtobwa, B.R. (2003),(Mh) Msalabani: *Siku Mia Moja na Hamsini za Mateso katika Maisha Yangu*, Heko Publishers Ltd, Dar es Salaam, Tanzania.

Ngugi.T. (2015), *Shetani Msalabani*, East African Education Publishers Ltd. Nairobi, Kenya.

Ntarangwi, N. (2004), *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*, Augustana College, Rock Island.

Oswald, E. E. (2005), "Writing in Hostile Space: A Critical Examination of South Afrikca Prison Literature", Thesis Submitted in Fulfilment on requirements of the degree of Doctor of Literatre and Phylosophy in English in The Fulculty of Arts, University of JohannesBurg, [Unpublished].

Shafi, A. (2003), *Haini*, Sasa Sema, Nairobi Kenya.

Tanzania Episcopal Conference. (2001), Haki za Wafungwa na Hali ya Magereza-Tanzania Bara, Ecoprint Ltd, Dar es Salaam, Tanzania.

TUKI. (2004), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Oxford University Press, Dar es Salaam, Tanzania.

Wafula na Njogu. (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, The Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Wamitila, K.W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*, Kenya Litho Ltd, Nairobi.

Wanjiru, K. (2010), "Prison Literature in East Africa", [Imepitiwa tarehe 02, Septemba, 2015, saa 3: 00 usiku), [https://kimaniwawanjiru.wordpress.com/].